


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**



**BUNGE LA TANZANIA**

---

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI KUHUSU UTEKELEZAJI WA  
MAJUKUMU YA WIZARA YA FEDHA NA OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI KWA MWAKA  
WA FEDHA 2025/2026 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA  
MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027**

---

*[Imetolewa chini ya Kanuni ya 121 (9) ya Kanuni za Kudumu  
za Bunge za Mwaka 2025]*

Ofisi ya Bunge,  
10 Barabara ya Morogoro,  
S.L.P 941,  
40490 Tambukareli,  
**DODOMA.**

2 Juni, 2026

**TAARIFA YA MAONI YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI KUHUSU  
UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA FEDHA KWA MWAKA 2025/26  
PAMOJA NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA  
WA FEDHA 2026/27**

---

**1.0. UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 121(1) ikisomwa pamoja na Kifungu cha 9 (a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za kudumu za Bunge za mwaka 2025 kinaipa Kamati jukumu la kusimamia Wizara ya Fedha. Aidha Kifungu cha 9(1)(c) cha Sheria ya Bajeti Sura 439 kinaipa Kamati jukumu la kupitia na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi. Kwa misingi hiyo, naomba kuwasilisha Taarifa ya maoni ya Kamati kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Fedha na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2025/26 na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2026/27.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilichambua na kujadili utekelezaji wa bajeti ya mafungu 8 ya Wizara ya fedha pamoja na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2025/26 pamoja na makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mafungu hayo kwa mwaka wa fedha 2026/27. Mafungu nane (8) ya Wizara ya Fedha pamoja na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ni kama ifuatavyo:-

- i. Fungu 050 – Wizara ya Fedha
- ii. Fungu 001 – Deni la Serikali
- iii. Fungu 006 – Idara ya Mkaguzi wa Ndani Mkuu wa Serikali
- iv. Fungu 010 – Tume ya pamoja ya Fedha
- v. Fungu 013 – Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu
- vi. Fungu 021 – Hazina

- vii. Fungu 022 – Huduma za Mfuko Mkuu
- viii. Fungu 023 – Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali
- ix. Fungu 045 – Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu sita ambazo ni:-

- i. Utangulizi;
- ii. Mapitio ya Utekelezaji wa majukumu na Bajeti ya Wizara ya Fedha pamoja na mafungu yaliyo chini yake kwa mwaka wa fedha 2025/26;
- iii. Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha pamoja na mafungu yaliyo chini yake kwa mwaka wa fedha 2026/27;
- iv. Mapitio ya utekelezaji wa bajeti ya Fungu 045 – Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa mwaka 2025/26 pamoja na uchambuzi wa makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2026/27;
- v. Maoni na Mapendekezo ya Kamati; na
- vi. Hitimisho.

## **2.0. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU NA BAJETI NA YA WIZARA YA FEDHA PAMOJA NA MAFUNGU YALIYO CHINI YAKE KWA MWAKA WA FEDHA 2025/26**

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2025/26 mafungu 8 ya Wizara ya Fedha yaliidhinishwa na Bunge jumla ya **shilingi trilioni 20,176,097,365,200.00**. Hadi kufikia Aprili, 2026 jumla ya **shilingi trilioni 14,083,113,444,713.4** zilipokelewa sawa na **asilimia 69.8** ya bajeti iliyoidhinishwa. Jedwali namba 1 linaonyesha utekelezaji wa bajeti ya mafungu hayo yaliyo chini ya Wizara ya Fedha hadi kufikia Aprili, 2026.

**Jedwali Na.1:Utekelezaji wa Bajeti ya Mafungu Nane (8) ya Wizara ya  
Fedha kwa mwaka wa fedha 2025/26**

<b>Fungu</b>	<b>Bajeti iliyoidhinishwa 2025/26</b>	<b>Fedha zilizotolewa hadi Aprili, 2026</b>	<b>Asilimia iliyoidhinishwa</b>
<b>001 Deni la Serikali</b>			
Matumizi Mengineyo	14,219,350,702,000	9,752,328,014,748.92	68.58
<b>Jumla Ndogo</b>	<b>14,219,350,702,000</b>	<b>9,752,328,010,000</b>	<b>68.32</b>
<b>006. Idara ya Mkaguzi wa Ndani Mkuu wa Serikali</b>			
Mishahara	2,366,512,000.00	1,894,976,799.00	80.07
Matumizi Mengineyo	11,430,429,000.00	10,286,556,166.31	89.99
Maendeleo ya Ndani	141,967,000.00	141,967,000.00	100
Maendeleo ya Nje	1,136,430,000.00	1,136,430,000.00	100
<b>Jumla Ndogo</b>	<b>15,075,338,000.00</b>	<b>13,459,929,965.31</b>	<b>89.28</b>
<b>010. Tume ya Pamoja ya Fedha</b>			
Mishahara	945,493,000.00	708,255,020.00	74.91
Matumizi mengineyo	4,164,536,000.00	3,285,145,234.67	78.88
Maendeleo	958,949,000.00	0	0
<b>Jumla Ndogo</b>	<b>6,068,978,000.00</b>	<b>3,993,400,254.67</b>	<b>65.80</b>
<b>013. Kitengo Cha Kudhibiti Fedha Haramu</b>			
Matumizi ya Kawaida	5,162,443,000.00	5,663,305,859.57	109.70
<b>Jumla Ndogo</b>	<b>5,162,443,000.00</b>	<b>5,663,305,859.57</b>	<b>109.70</b>
<b>021. Hazina</b>			
Mishahara	985,183,709,000.00	447,888,970,925.25	45.46
Matumizi mengineyo	783,658,931,000.00	1,158,493,173,913.24	147.83
Maendeleo Ndani	588,911,977,000.00	384,945,557,237.11	65.37
Maendeleo Nje	101,824,470,000.00	6,569,993,003.28	6.45
<b>Jumla Ndogo</b>	<b>2,459,579,087,000.00</b>	<b>1,997,897,695,078.83</b>	<b>81.23</b>
<b>022. Huduma za Mfuko Mkuu wa Serikali</b>			
Mishahara	16,616,460,000.00	9,253,260,270.20	55.69
Matumizi	3,131,303,648,000.00	2,024,354,493,991.27	64.65

<b>Fungu</b>	<b>Bajeti iliyoidhinishwa 2025/26</b>	<b>Fedha zilizotolewa hadi Aprili, 2026</b>	<b>Asilimia iliyoidhinishwa</b>
Mengineyo (Huduma za Mfuko Mkuu)			
<b>Jumla Ndogo</b>	<b>3,147,920,108,000.00</b>	<b>2,033,607,754,261.47</b>	<b>64.60</b>
<b>023. Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali</b>			
Mishahara	7,468,014,000.00	7,150,653,504	95.75
Matumizi Mengineyo	91,566,300,000	104,318,534,605	113.93
Maendeleo Ndani	741,381,000.00	741,381,000.00	100
Maendeleo Nje	4,090,081,000	2,456,788,000	60.07
<b>Jumla Ndogo</b>	<b>103,865,776,000.00</b>	<b>114,667,357,109.00</b>	<b>110.40</b>
<b>050. Wizara ya Fedha</b>			
Mishahara	89,011,587,000.00	75,272,903,317.28	84.57
Matumizi Mengineyo	80,571,827,200.00	64,829,083,244.98	80.46
Maendeleo Ndani	10,946,552,000.00	7,522,251,541.78	68.72
Maendeleo Nje	38,544,967,000.00	13,871,754,080.46	35.99
<b>Jumla Ndogo</b>	<b>219,074,933,200.00</b>	<b>161,495,992,184.50</b>	<b>73.72</b>
<b>Jumla kuu ya Bajeti</b>	<b>20,176,097,365,200.00</b>	<b>14,083,113,444,713.4</b>	<b>69.8</b>

**Chanzo:** Randama za Mafungu ya Wizara ya fedha

## **2.1. Uchambuzi wa Mafungu Nane (8)**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifanya uchambuzi wa Mafungu 8 na kubaini masuala yafuatayo:-

## **2.2. Fungu 01- Deni la Serikali**

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2025/26 Fungu hili liliidhinishwa kiasi cha **shilingi 14,219,350,702,000**. Hata hivyo katika kipindi cha nusu mwaka, yalifanyika mapitio ya bajeti na kubaini kiasi kinachohitajika kulipa deni ni **Shilingi 14,069,350,702**. Marejeo hayo yalisababisha na kushuka kwa mahitaji ya kulipa deni kwa **shilingi bilioni 150,000**, Kushuka huko kulitokana na

kuimarika kwa thamani ya shilingi dhidi ya baadhi ya sarafu za mataifa yanayotudai na kupungua kwa viwango vya riba vya marejeo vinavyotumika kimataifa vya SOFR (Secured Overnight Financing Rate) iliyotumika katika maandalizi ya bajeti. Kiasi hicho cha fedha kiliamishwa kwenye mafungu mengine yaliyokuwa na uhitaji wa fedha.

**Jedwali Na. 2: Mchanganuo wa Malipo ya Deni**

<b>Na</b>	<b>Mahitaji</b>	<b>Bajeti</b>	<b>Marejeo</b>	<b>Tofauti</b>
1.	Mtaji na Riba ya nje	7,186,133,824,000	6,479,184,371,000	706,949,453,000
2.	Mtaji na Riba ya ndani	7,022,844,678,000	7,569,720,049,000	(546,875,371,000)
3.	Kuhudumia Deni	10,202,200,000	20,276,282,000	(10,074,082,000)
4	Matangazo ya minada ya kuuza Dhamana	170,000,000	170,000,000	0
<b>5</b>	<b>JUMLA</b>	<b>14,219,350,702,000</b>	<b>14,069,350,702,000</b>	<b>(150,000,000,000)</b>

*Chanzo: Randama ya Fungu Namba 1*

**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Aprili, 2026, Fungu hili lilipokea jumla ya **Shilingi 9,752,328,010,000** sawa na **asilimia 69.32** ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya kiasi hicho **Shilingi 2,788,041,760,000** zilitumika kulipa mtaji na riba ya deni la nje, **Shilingi 2,270,026,240,000** zilitumika kulipa mtaji na riba ya deni la ndani, **shilingi 14,520,930,000** zilitumika kuhudumia deni na **Shilingi 92,300,000** zilitumika kugharamia matangazo ya minada ya kuuza dhamana za Serikali. Kamati inaipongeza Serikali inayoongozwa na **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** kwa kuwa na uwezo wa

kifedha wa kulipa madeni yetu kwa wakati na kama inavyostahiki.

**Mheshimiwa Spika**, Pamoja na kwamba Deni la Serikali ni himilivu kwa viwango vyote vya Kimataifa, kiashiria cha uwiano wa Deni kwa mauzo ya nje hivi sasa ni **asilimia 13.9** na ukomo ni **asilimia 15**. Hivyo edapo hatutaimarisha mauzo yetu nje na tunaweza kufikia ukomo na hivyo deni linaweza lisiwe himilivu. Kamati inaitaka Serikali kuwekeza kwenye sekta na mikakati inayoongeza mauzo nje ili kudhibiti deni na kuongeza thamani ya Shilingi. Aidha, Kamati inaitaka Serikali kupunguza ukopaji katika Soko la ndani ili kutoa fursa kwa Sekta Binafsi kupata mikopo na kwa riba nafuu.

### **2.3. Fungu 006 - Idara ya Mkaguzi wa Ndani Mkuu wa Serikali**

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2025/26 fungu 006 liliidhinishiwa kiasi cha **shilingi 15,075,338,000**. Kati ya kiasi hicho, shilingi **13,796,941,000** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **shilingi 1,278,397,000** ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Matumizi ya kawaida yanajumuisha **shilingi 2,366,512,000** kwa ajili ya mishahara na **shilingi 11,430,429,000** kwa ajili ya matumizi mengineyo. Aidha, kwa upande wa matumizi ya maendeleo kiasi cha **shilingi 141,967,000** ni fedha za ndani na **shilingi 1,136,430,000** ni fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Aprili, 2026 fungu 006 lilikuwa limepokea kiasi cha **shilingi 13,459,929,965.31** sawa na **asilimia 89.28** ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya kiasi hicho **shilingi 1,895,585,700.00** ni mishahara, **shilingi 10,286,556,166.31** ni matumizi mengineyo na **shilingi 1,278,397,000.00** ni fedha za maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa kuna changamoto ya kimuundo na kiutendaji ya Idara ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali pamoja na Wakaguzi wa Ndani. Changamoto hiyo inatokana na ukweli kwamba Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali anawajibika kiutendaji na kiutawala kwa Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mkaguzi wa Ndani anawajibika kiutawala na kiutendaji kwa afisa masuuli wa Taasisi husika. Hata hivyo, muundo huu umeonekana kuwa na changamoto ambapo Sheria ya ukaguzi wa umma Sura 418 haimpi mamlaka Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali kuwawajibisha wakaguzi wa ndani pindi wanapobainika kutenda makosa.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaendelea kuisisitiza Serikali kufanya mabadiliko ya kimuundo na kiutendaji ya Idara ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali pamoja na kutunga Sheria ya Ukaguzi wa Ndani ya Umma ili Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali awajibike kiutawala kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali na Taarifa yake ya Utendaji iwe inawasilishwa kwa Katibu Mkuu Kiongozi kupitia Kamati ya Ukaguzi ya Kitaifa (*The National Audit Committee*). Vilevile Sheria hii iweke masharti yatakayomfanya Mkaguzi Mkuu wa ndani kuwa huru. Aidha, kwakuwa fungu hili ndilo linahusika na ukaguzi wa madeni ya Wazabuni, Wakandarasi na Watoa huduma, Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha uhakiki unafanyika ndani ya siku 21 baada ya kupokea nyaraka ili kuondoa changamoto ya ucheleweshaji wa malipo kwa kigezo cha uhakiki.

#### **2.4. Fungu 10 – Tume ya Pamoja ya Fedha**

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2025/26 fungu 10 liliidhinishiwa kiasi cha **shilingi 6,068,978,000.00**. Kati ya kiasi hicho **shilingi 945,493,000** ni mishahara, **shilingi 4,164,536,00** ni matumizi

mengineyo na **shilingi 958,494,000** ni matumizi ya maendeleo. Hadi kufikia Aprili, 2026 fungu lilikuwa limepokea kiasi cha **shilingi 3,993,400,254.67** sawa na **asilimia 65.80** ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya kiasi kilichokuwa kimepokelewa, **shilingi 708,255,020.00** ni mishahara na **shilingi 3,285,145,234.67** ni matumizi mengineyo. Aidha, hakukuwa na fedha za maendeleo zilizopokelewa.

**Mheshimiwa Spika**, Tume hii inakabiliwa na changamoto kuu mbili, kama ifuatavyo:-

- i. Makamishna wa Tume kutoteuliwa kwa kipindi cha miaka saba (7) kuanzia mwaka 2019 jambo linaloathiri utekelezaji wa majukumu ya Tume;
- ii. Kuchelewa kwa ukamilishaji wa jengo la Ofisi ya Tume kwa Tanzania Bara;

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaendelea kumsisitiza Waziri wa Fedha kukumbusha Mamlaka ya uteuzi, kuteuwa Makamishna wa Tume ili kuwezesha Tume kutekeleza majukumu yake kikamilifu kwa mujibu wa lbara ya 133 ya Katiba ya Jamuhuri ya Muungano ya Mwaka 1977. Vilevile, Kamati inaitaka Tume kukamilisha ukarabati wa jengo hilo na kuhamia ifikapo Septemba, 2026.

## **2.5. Fungu 13 – Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu**

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2025/26 kitengo kiliidhinishwa kiasi cha **shilingi 5,162,443,000**. Hata hivyo baada ya uhamisho, bajeti ya fungu hili ilikuwa **shilingi 6,955,591,171** kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Hadi kufikia Aprili, 2026 Kitengo kilikuwa kimepokea kiasi cha **shilingi 5,663,305,859.5** kwa ajili ya matumizi ya kawaida sawa na **asilimia 109.7** ya bajeti iliyoidhinishwa.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilibaini kuwa Kitengo hiki bado kinakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

- i. Mabadiliko ya mara kwa mara ya mbinu za kihalifu katika masuala ya utakasishaji wa fedha haramu, ufadhili wa ugaidi na ufadhili wa silaha za maangamizi;
- ii. Ongezeko la Matumizi ya sarafu za kidigiti zinazotumika kutakatisha fedha; na
- iii. Matumizi ya fedha taslimu ambayo huchangia kwa kiasi kikubwa kutakatisha fedha haramu.

**Mheshimiwa Spika**, katika kukabiliana na changamoto hizo, Kamati inaitaka Serikali kukiwezesha kitengo kuwa mamlaka kamili yenye watumishi wake watakaowajibika kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ili kuongeza uwajibikaji na kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Aidha, Kamati inakishauri kitengo hiki katika utendaji kazi wake kisiwe kikwazo cha maendeleo kwa mtu mmoja mmoja na uchumi kwa ujumla.

## **2.6. Fungu 21 - Hazina**

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2025/26, Fungu 21 liliidhinishiwa jumla ya **shilingi 2,459,579,087,000** Kati ya fedha hizo, **shilingi 985,183,709,000** ni kwa ajili ya mishahara ikijumuisha bajeti ya marekebisho ya mishahara kwa watumishi wa umma na **shilingi 783,658,931,000** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na **shilingi 690,736,447,000** ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Hadi kufikia Aprili, 2026 Fungu hili limepokea jumla ya **shilingi 1,997,897,695,078.83** sawa na **asilimia 81.23** ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo, **shilingi 447,888,970,925.20** ni kwa ajili ya mishahara, **shilingi 1,158,493,173,913.24** ni fedha za matumizi mengineyo na **shilingi 391,515,550,240.39** ni fedha za maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, moja ya majukumu ya fungu 21 ni kusimamia mapato na matumizi ya fedha za Umma, kusimamia sera, sheria, kanuni na miongozo ya fedha, ununuzi wa umma, ubia kati ya sekta ya umma na binafsi pamoja na usimamizi wa Bajeti ya Serikali. Katika uchambuzi wa utekelezaji wa majukumu ya fungu hili, Kamati imebaini masuala yafuatayo:-

- i. Bado Matumizi yasiyo na tija yameendelea kuwepo katika mafungu mbalimbali ya Serikali;
- ii. Uchumi wetu kwa kiasi kikubwa unaendeshwa na matumizi ya Serikali ambapo ushirikishwaji wa Sekta Binafsi kwa njia ya Ubia ni hafifu na hivyo endapo mapato ya Serikali yatateteleka ni wazi kwamba tunaweza kuwa na msuko suko kwenye uchumi;
- iii. Maafisa masuuli kupanga Bajeti bila kuzingatia hali ya uchumi na hali ya upatikanaji wa fedha kwa Serikali;
- iv. Mafungu kuamini kuwa Hazina ina fedha za kutosha wao kutumia bila kuangalia makusanyo na mahitaji halisi ya Serikali;
- v. Maafisa masuuli kutofuata Sheria ya Bajeti na Sheria nyingine za kusimamia matumizi na kutekeleza miradi ya maendeleo;
- vi. Maafisa masuuli kuzalisha madeni kwenye manunuzi mbalimbali katika utekelezaji wa miradi na kutotoa kipaumbele katika ulipaji wake pindi wanapopata fedha;
- vii. Serikali kuuziwa bidhaa na huduma kwa bei ya juu kuliko gharama ya soko pamoja na kutumia mfumo wa kidijitali wa NeST kufanya manunuzi; na
- viii. Matumizi mabovu ya rasilimali za umma kama vile magari.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha kuwa inashughulikia changamoto hizo katika mwaka wa fedha

2026/27 na kuacha utaratibu wa kupanga Bajeti bila kuzingatia hali ya uchumi na upatikanaji wa fedha ifikapo mwaka 2027/28.

## **2.7. Fungu 22 – Huduma za Mfuko Mkuu wa Serikali**

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2025/26 Fungu hili liliidhinishiwa kiasi cha **shilingi 3,147,920,108,000.00**. Kati ya fedha hizo, **shilingi 16,616,460,000.00** ni kwa ajili ya mishahara ya maafisa wa umma wanaolipwa kupitia Fungu 022, na **shilingi 3,131,303,648,000.00** ni kwa ajili ya Huduma za Mfuko Mkuu. Hadi kufikia Aprili, 2026 jumla ya **shilingi 2,033,607,754,261.47** zimepokelewa sawa na **asilimia 64.60** ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo, **shilingi 9,253,260,270.2** ni mishahara na **shilingi 2,024,354,493,991.27** ni matumizi mengineyo.

**Mheshimiwa Spika**, fungu hili lina jukumu la kuandaa majibu ya hoja za ukaguzi zilizoibuliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Hata hivyo, taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya mwaka 2024/25 imebaini kuwa **asilimia 67** ya hoja zilizoibuliwa kwenye ripoti ya Serikali Kuu hazijafanyiwa kazi na kutolewa mrejesho na baadhi ya hoja ni za miaka 17-19. Kutofanyiwa kazi kwa hoja hizi imepelekea hoja nyingi kujirudia mara kwa mara na hivyo kuendelea kupunguza ufanisi wa matumizi wa fedha za umma pamoja na utekelezaji wa shughuli za Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia umuhimu wa kufanyia kazi hoja za ukaguzi katika kuimarisha na kuongeza ufanisi wa matumizi ya fedha za Umma, Kamati inaitaka Serikali kupitia fungu hili kuhakikisha inafuatilia na kuandaa majibu ya hoja za ukaguzi ili Bunge liweze kuishauri Serikali. Aidha, Taarifa hiyo iwe inawasilishwa kwenye Kamati ya PAC na LAC ambao kwa mujibu wa kanuni wataleta mrejesho wa utekelezaji wake

Bungeni. Vilevile, Kamati inalishauri Bunge kwamba mapendekezo yaliyowasilishwa Serikalini kwa ajili ya kuchukua hatua za kinidhamu kwa wabadilifu yabainishe ni nani muhusika na hatua zipi zichukuliwe ili kuleta uwajibikaji na nidhamu ya fedha za Umma. Hali ilivyo hivi sasa mapendekezo mengi yanapelekwa Serikalini kiujumla na hivyo kutoa mwanya wa lipi lifanyiwe kazi kwanza.

## **2.8. Fungu 23 - Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali**

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2025/26, Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali iliidhinishiwa kiasi cha **shilingi 103,865,776,000**. Kati ya fedha hizo, **shilingi 7,468,014,000** ni kwa ajili ya Mishahara kwa watumishi wa Idara, **shilingi 91,566,300,000** kwa ajili ya matumizi mengineyo na **shilingi 4,831,462,000** ni fedha za maendeleo. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2026 Idara ilipokea kiasi cha **shilingi 114,667,357,109** sawa na **asilimia 110.40** ya bajeti ya iliyoidhinishwa. Kati ya kiasi hicho, **shilingi 7,150,653,504** ni kwa ajili ya mishahara, **shilingi 104,318,534,605** kwa ajili ya matumizi mengineyo na **shilingi 3,198,169,000** ni kwa ajili ya maendeleo. Ufanisi wa utekelezaji wa bajeti ulitokana na nyongeza ya bajeti ya matumizi ya kawaida ya **shilingi 39,180,000,000** na hivyo kuifanya bajeti ya matumizi ya kawaida kufika kiasi cha **shilingi 138,214,314,000**.

**Mheshimiwa Spika**, moja ya jukumu la fungu hili ni kusimamia Mfuko Mkuu wa Serikali, mifuko maalum, mifuko ya pamoja (basket funds), Akaunti Jumuiifu ya Hazina na akaunti mbalimbali za amana. Kamati imefanya uchambuzi kuhusu mwenendo wa uwasilishaji wa makusanyo kwenye mifuko maalumu iliyolindwa na kubaini kwamba kwa mujibu wa Kifungu cha 41(2)(a) cha Sheria ya Bajeti Sura 439, kinaweka katazo kwa Afisa Masuuli kufanya uhamisho wa fedha zilizoidhinishwa kwa matumizi ya

Mifuko Maalum yenye vyanzo vilivyolindwa. Hata hivyo mifuko hii bado imeendelea kukabiliwa na changamoto zifuatazo:-

- i. Bajeti ya mifuko kutengwa chini ya makusanyo halisi.
- ii. Fedha zinazowasilishwa kwenye mifuko kutokana na makusanyo kuwa chini ya kiasi kilichokusanywa kutokana na changamoto za ukwasi kwenye mfuko mkuu; na
- iii. Matumizi ya fedha zilizopo kwenye akaunti za mifuko kuhitaji idhini ya Mlipaji Mkuu wa Serikali ili zitumike jambo ambalo limekuwa linasababisha kuchelewa kutekeleza miradi iliyoko chini ya mifuko hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia malengo ya kuanzisha mifuko hiyo maalum ni kuwa na uhakika wa rasilimali fedha za kutekeleza miradi muhimu ya Reli, Bandari, Barabara, Maji na Mawasiliano. Hivyo, Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) inapokusanya mapato kutoka vyanzo mahususi kuyawasilisha kwenye mifuko husika moja kwa moja. Hatua hii itasaidia kuondokana na changamoto hizo ili kuwezesha fedha za mifuko kutumika kama ilivyokusudiwa. Aidha fedha zilizoko kwenye akaunti za mifuko zitumike kwa malengo yaliyokusudiwa kwa utaratibu rahisi.

## **2.9. Fungu 50 - Wizara ya Fedha**

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2025/26, Fungu hili liliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 219,074,933,200.00** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo. Kati ya kiasi hicho, **shilingi 89,011,587,000.00** ni kwa ajili ya mishahara, **shilingi 80,571,827,200.00** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **shilingi 49,491,519,000.00** ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo kwa Idara, Vitengo na Taasisi zilizo chini ya Fungu hili.

**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Aprili, 2026 jumla ya **shilingi 161,495,992,184.50** zimetolewa sawa **asilimia 73.72** ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo **shilingi 75,272,903,317.28** ni mishahara, **Shilingi 64,829,083,244.98** ni matumizi mengineyo, **shilingi 21,394,005,622.24** ni fedha za maendeleo. Aidha, uchambuzi wa Kamati ulibaini bajeti ya matumizi mengineyo ilifanyiwa marekebisho kwa kupunguza kiasi cha **shilingi 1,203,920,000** hivyo kufanya bajeti hiyo kufikia kiasi cha **shilingi 78,437,085,200** kutoka **shilingi 79,641,005,200** iliyoidhinishwa.

**Mheshimiwa Spika**, fungu hili linahusika na kubuni na kusimamia mifumo ya kieletroniki ya usimamizi wa fedha na TEHAMA pamoja na kuratibu utekelezaji wa programu ya maboresho ya usimamizi wa Fedha za Umma. Hata hivyo, kumekuwa na changamoto katika usimamizi wa fedha za umma, ambapo baadhi ya fedha hazitumiki kama ilivyokusudiwa na hivyo kuathiri utekelezaji wa bajeti hasa kwenye miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha fedha zinatumika kama ilivyoidhinishwa ili kuleta matokeo yaliyokusudiwa kwa kuendelea kuboresha mifumo pamoja na programu za usimamizi wa fedha za umma. Aidha, sambamba na jukumu hili Serikali kupitia fungu hili liendeleo kuimairisha usimamizi wa vihatarishi vinavyoweza kuathiri utekelezaji wa bajeti ili kuhakikisha bajeti inatekelezwa kama ilivyokusudiwa.

**3.0. UCHAMBUZI WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA FEDHA PAMOJA NA MAFUNGU YALIYO CHINI YAKE KWA MWAKA WA FEDHA 2026/27**

**3.1. Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mafungu nane (8) ya Wizara ya Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2026/27**

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2026/27, Wizara ya Fedha pamoja na mafungu yaliyo chini yake inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Shilingi 21,335,984,722,000** sawa na ongezeko la **asilimia 5.75** kutoka bajeti ya **Shilingi 20,176,097,365,200.00** mwaka 2025/26. Kati ya kiasi kinachoombwa, **Shilingi 14,712,796,574,000** ni kwa ajili ya ulipaji wa Deni, **Shilingi 19,446,887,571,000** ni kwa ajili ya matumizi kawaida na **Shilingi 1,889,097,151,000** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Jedwali namba 3 linaonyesha mchanganuo wa maombi ya fedha kwa Wizara ya Fedha na Mafungu yaliyo chini yake kwa mwaka wa fedha 2026/27.

**Jedwali Na. 3: Maombi ya Fedha kwa Wizara ya Fedha na Mafungu yaliyo chini yake kwa mwaka wa fedha 2026/27**

Fungu	Matumizi Mengineyo	Mishahara	Miradi Maendeleo ya (Ndani)	Miradi Maendeleo ya (Nje)	Jumla
1	14,712,796,574,000	-	-	-	14,712,796,574,000
6	11,487,386,000	2,504,376,000	141,967,000	1,000,000,000	15,133,729,000
10	4,164,536,000	957,619,000	958,949,000	-	6,081,104,000
13	5,162,443,000	-	-	-	5,162,443,000
21	655,093,785,000	656,617,043,000	1,482,162,535,000	217,320,607,000	3,011,193,970,000
22	3,126,051,357,000	22,586,628,000			3,148,637,985,000
23	70,209,670,000	9,006,648,000	3,241,381,000	3,000,000,000	85,457,699,000
50	76,741,433,000	93,508,073,000	14,100,752,000	167,170,960,000	351,521,218,000
<b>Jumla</b>	<b>18,661,707,184,000</b>	<b>785,180,387,000</b>	<b>1,500,605,584,000</b>	<b>388,491,567,000</b>	<b>21,335,984,722,000</b>

**Chanzo:** Randama za Mafungu ya Wizara ya Fedha

### 3.2. Uchambuzi wa baadhi ya Mafungu

**Mheshimiwa Spika**, baada ya uchambuzi wa mafungu 8, Kamati ilibaini na kupendekeza masuala yafuatayo:-

#### a) Fungu 13 – Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2026/27 kitengo hiki kimepanga Kuunda mfumo wa TEHAMA utakaounganishwa na taasisi za kifedha kwa ajili ya kurahisisha upatikanaji na uchakataji wa taarifa za utakatishaji wa fedha haramu, ufadhili wa ugaidi na ufadhili wa silaha za maangamizi. Hata hivyo bado kumekuwa na changamoto mbalimbali katika mifumo ya Serikali kama vile mifumo kutosomana na mifumo kutofanya kazi kikamilifu kutokana na ukosefu wa mtandao au kuzidiwa. Hali hii itapelekea mfumo utakao undwa na kitengo kushindwa kupata na kuchakata taarifa za utakatishaji fedha haramu.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati kuhakikisha kwamba katika utekelezaji wa Bajeti kabla ya nusu mwaka fungu hili liongezewe jumla ya shilingi **3,711,120,000** ili kutekeleza shughuli mbalimbali za kitengo ikiwemo kuimarisha mifumo na kuhakikisha inasomana ili kudhibiti vitendo vya utakatishaji fedha, ufadhili wa ugaidi na ufadhili wa silaha za maangamizi.

#### b) Fungu 021 – Hazina

**Mheshimiwa Spika**, Misamaha ya kodi ni nyenzo muhimu inayotumiwa na Serikali katika kuchochea uwekezaji, kupunguza gharama kwa wananchi na kuendeleza sekta za kimkakati. Hata hivyo, utekelezaji wake umekuwa na changamoto kadhaa zinazohitaji maboresho ili kuhakikisha

misamaha hiyo inaleta matokeo chanya kwa uchumi wa taifa. Changamoto hizo ni kama ifuatavyo:-

- i. Baadhi ya misamaha hutolewa kwa sekta zisizo na mchango mkubwa katika uchumi;
- ii. Hakuna ufuatiliaji thabiti ili kubaini endapo misamaha iliyotolewa inaleta matokeo yaliyokusudiwa;
- iii. Imekuwa ikipunguza mapato ya ndani na kuongeza utegemezi wa mikopo na misaada; na
- iv. Imekuwa ikitumiwa vibaya na baadhi ya wawekezaji.

**Mheshimiwa Spika**, katika kutatua changamoto hizo, Serikali inatarajia Kuandaa mapendekezo ya kutunga Sheria ya Misamaha ya Kodi katika mwaka wa fedha 2026/27. Kamati inaishauri Serikali kuweka matakwa yafuatayo katika Sheria hiyo:-

- i. Kuelekeza msamaha kwa Sekta za Kimkakati zinazochangia ajira na ukuaji wa Uchumi kama vile kilimo, viwanda vidogo, nishati mbadala, na teknolojia; na
- ii. Kufanya tathmini kila mwaka ya athari za misamaha ya kodi kwa mapato ya serikali.

c) **Fungu 50 – Wizara ya Fedha**

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2026/27, moja ya vipaumbele vya Fungu 50 ni kutunga Sera ya Usimamizi wa Mali za Umma na mkakati wa utekelezaji wake. Hata hivyo kumekuwa na changamoto mbalimbali katika usimamizi wa mali za umma kama vile kutokuwepo kwa mpango madhubuti wa matengenezo ya mali, ukosefu wa hatimiliki za baadhi ya mali, kuwepo kwa mali zilizotelekezwa hali inayopelekea mali za umma kuwa katika hatari ya kuvamiwa na kutumika vibaya na hivyo kulisababishia Taifa hasara.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaitaka Serikali kuharakisha utungaji wa Sera hiyo pamoja na mkakati wake wa utekelezaji wa Sera ya Usimamizi ili mali za umma zitumike kwa ufanisi na kuwa salama.

#### **4.0. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI- FUNGU 045 KWA MWAKA WA FEDHA 2025/26 PAMOJA NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/27**

**Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ina jukumu la kufanya ukaguzi wa mapato na matumizi ya Serikali, kama yalivyoidhinishwa na Bunge. Majukumu mengine ya Ofisi hiyo ni kama yafuatayo:-

- i. Kukagua Hesabu za Wizara, Mikoa, Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa na Majiji, Ofisi za Balozi za Tanzania zilizopo nje ya nchi, Wakala za Serikali, Mashirika ya Umma, pamoja na miradi ya Maendeleo inayogharamiwa na wafadhili na kutoa taarifa ya ukaguzi wa mapato na matumizi ya fedha za umma Bungeni;
- ii. Kujenga, kukuza na kuimarisha utamaduni wa uwajibikaji katika Wizara, Taasisi za Serikali, Mikoa na Halmashauri;
- iii. Kuhakikisha kwamba, inajiridhisha uwepo wa uwajibikaji wa kutosha katika kusimamia na kudhibiti ipasavyo ukusanyaji wa mapato na matumizi ya Serikali; na
- iv. Kuhakikisha kuwa jamii ya Tanzania inapata faida au tija kutokana na matumizi bora ya fedha za umma, na mali za umma zinahifadhiwa, kutunzwa na kulindwa ipasavyo.

#### **4.1. Mwenendo wa utolewaji wa Fedha kwa fungu 45 kwa mwaka wa Fedha 2025/26**

**Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2025/26 iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 123,362,123,000**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 23,058,129,000** ni kwa ajili ya mishahara,

**Shilingi 87,356,994,000** kwa ajili ya matumizi mengineyo na **Shilingi 12,103,996,000** kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Aidha, Fungu hili lilipangiwa kukusanya maduhuli yenye jumla ya **Shilingi 843,004,000**. Hadi mwezi Aprili, 2026 Fungu limepokea jumla ya **Shilingi 99,079,159,647** sawa na **asilimia 87.89** ya bajeti yote. Kamati inampongeza **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** kwa kuhakikisha Fungu hili linapata fedha za kutosha kwa ajili ya kuwezesha ofisi hii kutekeleza majukumu yake ya kikatiba ya udhibiti na ukaguzi. Mchanganuo wa utolewaji wa fedha ni kama unavyoonekana kwenye **jedwali namba 3** hapo chini.

**Jedwali Na. 4: Utekelezaji wa Bajeti ya Fungu 45 Hadi Kufikia Aprili, 2026.**

<b>Aina ya Matumizi</b>	<b>Bajeti iliyoidhinishwa 2025/26</b>	<b>Fedha iliyotolewa hadi Aprili 2026</b>	<b>Asilimia</b>
Mishahara	23,058,129,000	18,025,524,640	78.2
Matumizi Mengineyo	87,356,994,000	91,867,495,000	105.2
Maendeleo Ndani	8,828,000,000	6,783,535,025	76.8
Maendeleo Nje	3,275,996,000	2,243,250,000	68.5
<b>Jumla</b>	<b>122,519,119,000</b>	<b>118,919,804,665</b>	<b>97.1</b>

**Chanzo: Randama ya Fungu 45, 2026**

**4.2. Masuala ya Msingi yaliyobainika katika Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.**

**4.2.1. Mafanikio ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi katika mwaka 2025/26**

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2025/26 ofisi imefanikiwa kufanya yafuatayo:-

- i. Kufanya kaguzi 1,626 za mapato na matumizi chini ya Serikali Kuu, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa na Mashirika ya Umma;

- ii. Kukamilishaji Ripoti Kuu sita (6) za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali zilizowasilishwa kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 30 Machi, 2026;
- iii. Kuendeleza ujenzi wa Mfumo wa Uvunaji wa Taarifa za Fedha (ADLS) awamu ya tatu kwa ajili ya ukaguzi wa mapato na matumizi ya Serikali;
- iv. Kutoa mafunzo kwa Watumishi 630 kuhusu nyanja mbalimbali za ukaguzi;
- v. Kukamilisha ujenzi wa majengo ya Ofisi katika Mikoa ya Kilimanjaro na Dar es Salaam;
- vi. Kuanza ujenzi wa jengo la kwanza la kituo cha mafunzo cha ukaguzi (National Audit Academy – NAA) kwa lengo la kuwa na mazingira bora ya kujifunzia masuala ya ukaguzi kwa wakaguzi na wadau wa Ofisi;
- vii. Uanzishaji wa program za mafunzo kupitia Kituo cha Mafunzo cha Ofisi (National Audit Academy – NAA) ambapo mafunzo ya awali yameendelea kutolewa kwa njia ya mtandao (Online);
- viii. Kuwajengea uwezo Wajumbe 84 wa Kamati za Kudumu za Bunge za Usimamizi wa Fedha (LAAC, PAC, PIC na PBC); na
- ix. Kuendelea na za ujenzi wa Ofisi za Ukaguzi katika mikoa ya Mwanza na Ruvuma.

#### **4.2.2. Changamoto za Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi katika mwaka 2025/26**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kwamba Fungu hili linakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

- i. Kuongezeka kwa maeneo mapya ya ukaguzi kutokana na kuongezeka kwa shughuli za Serikali

hivyo kuhitaji ujuzi kupitia mafunzo mbalimbali na rasilimali fedha;

- ii. Ushirikishwaji wa Ofisi usioridhisha wakati wa uanzishwaji wa Mifumo mbalimbali inayotumiwa Serikalini;
- iii. Mabadiliko ya mara kwa mara ya Miongozo na viwango vya ukaguzi na uaandaaji wa taarifa za fedha inayopelekea kuongezeka kwa mahitaji makubwa ya fedha kwa ajili ya kuwajengea uwezo wakaguzi na kuhuisha miongozo ya ndani ya ukaguzi;
- iv. Mishahara ya watumishi wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kutofanyiwa mapitio kwa muda mrefu;
- v. Mahitaji endelevu ya vitendea kazi hususani kompyuta 206, printa 14, magari 6 na mazingira bora ya kazi; na

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Serikali kuendelea kuongeza fedha kwa Fungu 45 ili ofisi iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

#### **4.3. Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa Mwaka wa Fedha 2026/27**

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2026/27 Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi inatarajia kukamilisha utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Miaka Mitano (2021/22 – 2025/26) uliorejewa mwaka 2023/24 ambao unajielekeza katika kuimarisha kazi za ukaguzi wa Sekta ya Umma nchini. Kimsingi, Ofisi imelenga kutekeleza vipaumbele vifuatavyo:-

- i. Ukaguzi wa mapato na matumizi ya Serikali, ukaguzi wa Ufanisi, ukaguzi wa Kiufundi, ukaguzi wa Mifumo, ukaguzi

- wa Kiuchunguzi pamoja na ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo;
- ii. Kuwajengea uwezo watumishi katika maeneo mbalimbali ya kiukaguzi na kiutendaji;
  - iii. Uimarishaji wa matumizi ya mifumo ya TEHAMA, upatikanaji wa vitendea kazi, ujenzi na ukarabati wa majengo ya Ofisi za Ukaguzi ili kuongeza tija na ufanisi katika utendaji kazi;
  - iv. Kuzijengea uwezo Kamati za Kudumu za Bunge za Usimamizi katika kuelewa Majukumu, Mamlaka ya CAG, Uchambuzi wa ripoti za CAG na Utambuzi wa mbinu za kufanya ufuatiliaji wa matumizi ya fedha za utekelezaji wa shughuli mbalimbali za maendeleo;
  - v. Kutenga nafasi za kuajiri watumishi katika maeneo yenye uhitaji;
  - vi. Kuendelea na ujenzi katika mikoa ya Ruvuma, Mwanza, Tanga na Mtwara; ukarabati wa Ofisi za Ukaguzi katika mikoa mbalimbali na uendelezaji ujenzi wa Kituo cha Mafunzo cha Ukaguzi (National Audit Academy); na
  - vii. Usimamizi mahsusi wa utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya Taifa 2050.

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2026/27 Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi imetengewa jumla ya **Shilingi 132,224,661,000**. Kati ya fedha hizo **Shilingi 120,396,661,000** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida, **Shilingi 8,828,000,000** ni fedha za ndani za maendeleo na **Shilingi 3,000,000,000** ni fedha za nje. Aidha, Fungu limeidhinishiwa kukusanya Maduhuli yenye jumla ya **Shilingi 485,334,000** kwa ajili ya kwenda Mfuko Mkuu wa Serikali.

**Jedwali Na. 5: Ulinganisho wa Bajeti ya NAOT kwa Mwaka wa fedha 2025/26 Na Makadirio ya Bajeti Kwa Mwaka wa fedha 2026/27.**

<b>Maelezo</b>	<b>Bajeti iliyoidhinishwa (2025/26)</b>	<b>Makadirio ya Mwaka (2026/27)</b>	<b>Tofauti (2026/27-2025/26)</b>	<b>Asilimia (2026/27-2025/26)</b>
Maduhuli	843,004,000	485,334,000	-357,670,000	-42.43
<b>Jumla ya fedha za Maduhuli</b>	<b>843,004,000</b>	<b>485,334,000</b>	<b>-357,670,000</b>	<b>-42.43</b>
<b>Matumizi ya Kawaida</b>				
Mishahara	23,058,129,000	23,939,667,000	881,538,000	3.82
Matumizi Mengineyo	87,356,994,000	96,456,994,000	9,100,000,000	10.42
<b>Jumla ya matumizi ya kawaida</b>	<b>110,415,123,000</b>	<b>120,396,661,000</b>	<b>9,981,538,000</b>	<b>9.04</b>
<b>Matumizi ya Maendeleo</b>				
Fedha za ndani	8,828,000,000	8,828,000,000	0	0.00
Fedha za Nje	3,275,996,000	3,000,000,000	-275,996,000	-8.42
<b>Jumla ya fedha za Maendeleo</b>	<b>12,103,996,000</b>	<b>11,828,000,000</b>	<b>-275,996,000</b>	<b>-2.28</b>
<b>Jumla Kuu</b>	<b>123,362,123,000</b>	<b>132,709,995,000</b>	<b>9,347,872,000</b>	<b>7.58</b>

*Chanzo: Randama ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, 2026*

**4.4. Maombi ya Fedha ya Wizara ya Fedha pamoja na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa Mwaka wa Fedha 2026/27**

**Mheshimiwa Spika**, jumla ya fedha zote zinazombwa na Mafungu nane (8) ya Wizara ya Fedha pamoja na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa Mwaka 2026/27 ni Shilingi **21,468,209,383,000**. Kati ya fedha hizo, Shilingi **19,567,284,232,000** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida, Shilingi **1,900,925,151,000** ni kwa ajili ya fedha za miradi ya maendeleo.

**Jedwali Na. 6: Maombi ya Fedha kwa Wizara ya Fedha na Mafungu yaliyochini yake kwa mwaka 2025/26**

<b>Fungu</b>	<b>Matumizi Mengineyo</b>	<b>Mishahara</b>	<b>Miradi ya Maendeleo (Ndani)</b>	<b>Miradi ya Maendeleo (Nje)</b>	<b>Jumla</b>
01	14,712,796,574,000	-	-	-	14,712,796,574,000
06	11,487,386,000	2,504,376,000	141,967,000	1,000,000,000	15,133,729,000
10	4,164,536,000	957,619,000	958,949,000	-	6,081,104,000
13	5,162,443,000	-	-	-	5,162,443,000
21	655,093,785,000	656,617,043,000	1,482,162,535,000	217,320,607,000	3,011,193,970,000
22	3,126,051,357,000	22,586,628,000			3,148,637,985,000
23	70,209,670,000	9,006,648,000	3,241,381,000	3,000,000,000	85,457,699,000
50	76,741,433,000	93,508,073,000	14,100,752,000	167,170,960,000	351,521,218,000
<b>Jumla</b>	<b>18,661,707,184,000</b>	<b>785,180,387,000</b>	<b>1,500,605,584,000</b>	<b>388,491,567,000</b>	<b>21,335,984,722,000</b>
45	96,456,994,000	23,939,667,000	8,828,000,000	3,000,000,000	132,224,661,000
<b>JUMLA KUU</b>	<b>18,758,164,178,000</b>	<b>809,120,054,000</b>	<b>1,509,433,584,000</b>	<b>391,491,567,000</b>	<b>21,468,209,383,000</b>

**Chanzo: Randama za Mafungu ya Wizara ya Fedha na Ofisi ya CAG, 2026**

**5.0. MAONI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

**Mheshimiwa Spika**, baada ya Kamati kupitia utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Fedha na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2025/26 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2026/27, Kamati ina maoni na Mapendekezo yafuatayo:-

**5.1. Kuanzisha sera ya benki ya maendeleo pamoja na kufanya mapitio ya muundo na uendeshaji wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB)**

**Mheshimiwa Spika**, Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) ilianzishwa kwa lengo la kuwa ni benki ya maendeleo ya kilimo kwa dhana ya kupatikana mikopo nafuu na ya muda mrefu ili kuleta mapinduzi ya sekta ya kilimo nchini. Kwa sasa Benki hii ina mtaji wa **shilingi bilioni 452.4**. Tangu kuanzishwa kwake, imekuwa ikitoa mikopo kama benki ya kibiashara

(commercial bank) na kusimamiwa na sera na sheria zinazoongoza sekta ya fedha kibiashara. Aidha TADB pamoja na changamoto hiyo imeendelea kutoa mikopo ya kibiashara kwa riba isiyoziidi **asilimia 10** jambo ambalo ni kinyume na lengo la uanzishwaji wake. TADB imetoa zaidi ya shilingi **trilioni 1.38** katika mikopo ya kilimo. Kati ya mikopo hiyo, **shilingi trilioni 1.15** zilitolewa kama mikopo ya moja kwa moja na **shilingi bilioni 496.12** kupitia Mfuko wa Dhamana ya Mikopo kwa Wakulima Wadogo (SCGS). Aidha TADB imewafikia wanufaika **3,245,531** kupitia mikopo ya kilimo.

**Mheshimiwa Spika**, licha ya mafanikio hayo, Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) bado haijawafikia wakulima wengi wadogo na wakubwa kutokana na changamoto zifuatazo:

- i. TADB kuendelea kutoa mikopo ambayo ni ghali na ya muda mfupi isiyoendana na dhana ya uanzishwaji wake na kujikita zaidi kuendeshwa, kusimamiwa kama benki ya biashara.;
- ii. TADB ina upungufu mkubwa wa mtaji jambo ambalo linahitaji hatua madhubuti na za haraka ili kuendana na malengo ya Dira 2050 ikiwemo kufanyika tathmini ya haraka kuunganisha TADB na benki ya uwekezaji (TIB) ili kuwa na benki moja kubwa ya maendeleo ya kilimo na viwanda pamoja na kutafuta wabia wa kimataifa na kuirodhesha kwenye soko la hisa. Hatua hizo zitaaidia benki hii kutimiza lengo la uanzishwaji wake;
- iii. Ukosefu wa sera na sheria ya kusimamia benki ya maendeleo, sera ya ukopeshaji wa sekta za uzalishaji hasa kilimo (Agricultural Financing Policy); na
- iv. Kuongezeka kwa mikopo chechefu kutokana na gharama kubwa ya mikopo, muda mfupi wa kulipa, kutokuwepo

kwa mfuko wa dhamana wa kulinda anguko la bei ya mazao ya wakulima, kutokuwepo kwa mfumo bora wa bima unaokinga hasara za wakulima kwenye uzalishaji, uhifadhi na sokoni. Hasara hizi zinaisababishia Benki kuwa na kiasi kikubwa cha mikopo chechefu.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Serikali kuanzisha sera ya benki ya maendeleo, kufanya mapitio ya sera ya maendeleo ya viwanda pamoja na kufanya mapitio ya kina ya muundo na uendeshaji wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) ili ijiendeshe kama Benki ya Maendeleo na si kama ilivyo hivi sasa. Hatua hiyo, itawezesha Benki hiyo kutekeleza majukumu yake kikamilifu ya kutoa dhamana, mitaji nafuu na ya muda mrefu kama benki ya maendeleo badala ya kuendelea kufanya kazi kama Benki ya biashara.

## **5.2. Kuanzishwa kwa sera mahsusni ya ufadhili wa sekta ya kilimo (agricultural financing policy)**

**Mheshimiwa Spika**, kwa kutambua kwamba Wizara ya Fedha ndiyo inayosimamia sera za fedha, sasa ni wakati muafaka wa kuanzisha sera ya ugharamiaji wa sekta ya kilimo. Aidha, Sekta ya Kilimo imeendelea kuongoza kwa kuwa na mchango mkubwa kwenye Pato la Taifa kwa **asilimia 26.3**. Sekta hii imekuwa ikitekeleza miradi mbalimbali ya kimkakati ukizingatia kuwa zaidi ya **asilimia 60** ya watanzania wanajishughulisha na kilimo.

**Mheshimiwa Spika** Sekta hii imekuwa ikikabiliwa na changamoto kubwa ya upatikanaji wa mitaji mfano, mikopo yote iliyoingia kwenye uchumi kwa kipindi cha mwaka mmoja ni zaidi ya **shilingi trilioni 40**, ambapo sekta ya kilimo ilipokea kiasi cha

**shilingi trilioni 4** sawa na wastani usiozidi **asilimia 10** ya mikopo yote.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaitaka Serikali kuanzisha sera mahsusi ya ugharamiaji kwa sekta ya kilimo, mifugo, misitu na uvuvi (agricultural finance policy) ambayo itasaidia ukuaji wa sekta hizi za uzalishaji na kuchochea viwanda.

### 5.3. **Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP)**

**Mheshimiwa Spika**, Dira ya Maendeleo ya Taifa ya 2050 imeweka wazi kuwa *Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP)* ni nguzo muhimu ya utekelezaji wa malengo ya taifa. Dira inasisitiza kuwa sekta binafsi ndiyo injini ya ukuaji wa uchumi, na PPP ni chombo cha kuhakikisha sekta binafsi inashiriki kikamilifu katika miradi ya maendeleo ya kitaifa. Kamati inatambua kuwa PPP ni mkakati wa lazima wa kufanikisha maendeleo ya taifa. Kupitia PPP, Tanzania itaweza kuhamasisha mitaji, kuimarisha sekta binafsi, kupunguza mzigo wa mahitaji ya fedha kwa Serikali ili kufanikisha utekelezaji wa miradi mikubwa ya kitaifa kwa uwazi na uwajibikaji.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa Wizara ya Fedha kupitia kituo cha Ubia inasimamia masuala yote na miradi inayohusu PPP, Kamati ilikuwa na maoni yafuatayo:

- i. Wizara ya Fedha kuzitaka Mamlaka zote za Serikali kuwa kila mwaka zinaandaa na kutekeleza miradi kwa njia ya PPP na pale itakapokuwa inabidi Wizara isitoe fedha za Serikali kwa miradi ambayo inaweza kutekelezwa kwa njia ya ubia;
- ii. Ili PPP iwe na tija kuna umuhimu wa Serikali kuweka mifumo madhubuti ya uwajibikaji na ufuatiliaji. Miradi ya PPP inahitaji mifumo thabiti ya kisheria na kiutendaji ili kuhakikisha miradi inatekelezwa kwa uwazi, na maslahi ya wananchi

yanalindwa. Hivyo, Kamati inasisitiza umuhimu wa usimamizi thabiti wa mikataba ya PPP ili kuepuka hatari za kifedha zinazoweza kujitokeza;

- iii. Kubadili mtazamo wa Watumishi wa Umma kwamba miradi yote lazima itekelezwe na Serikali: na
- iv. Kuangalia uwezekano wa kubadili hadhi ya Kituo cha Ubia (PPP Center) kuwa Mamlaka ya Ubia Baina ya Sekta binafsi (PPP Authority).

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaamini masuala hayo yakifanyiwa kazi tutaanza kuona utekelezaji wa miradi kwa njia ya PPP.

#### **5.4. Ufunguaji wa masoko ya mitaji (Capital Markets Liberalization)**

**Mheshimiwa Spika**, moja ya mipango ya Serikali ya Dira ya Maendeleo ya Taifa ya 2050 ni pamoja na kufungua soko la mitaji kwa wawekezaji wa nje na ndani ya nchi (capital liberalization) ifikapo mwaka 2027. Hatua ya Serikali ya kufungua masoko ya mitaji ni sera yenye manufaa makubwa kwa uchumi, hususan katika kuvutia mitaji ya kimataifa na kuongeza uwekezaji wa moja kwa moja wa kigeni (FDI), kufungua uchumi kwa mitaji ya kimataifa, kuboresha uwazi, uwajibikaji na sera za fedha. Hata hivyo ili Serikali iweze kunafikiwa katika hili masuala yafuatayo yanapaswa yazingatiwe:

- i. **Kusimamia sera na kanuni za fedha;** kufungua masoko ya mitaji inahitaji sera thabiti na kanuni madhubuti za kifedha ili kupunguza hatari za mtikisiko wa soko na kuhakikisha uwajibikaji. Hivyo, Wizara ya Fedha kupitia Hazina inapaswa kuandaa miongozo ya kina ya ufuatiliaji wa mtiririko wa mitaji. Ikiwemo kusimika mifumo ya kuweza kutambua mapema vihatarishi (early warning systems). Aidha, utafiti uliofanywa na IMF (2024) imeonyesha kuwa kuwa nchi

zinazoimarisha mifumo ya ufuatiliaji wa mitaji hupunguza hatari za kutoroshwa kwa mitaji (capital flight) kwa zaidi ya **asilimia 40**.

- ii. **Usimamizi thabiti wa deni la Serikali;** Ufunguaji wa masoko ya mitaji kunatoa fursa ya kupata mikopo nafuu kupitia hatifungani za makampuni (corporate bonds). Hazina inapaswa kuhakikisha kuwa mikopo hii inatumika kwa miradi yenye tija na si kuongeza mzigo wa deni lisilo na faida. Ripoti ya Benki ya Maendeleo ya Afrika ya mwaka 2022 (AfDB, 2022) inaonyesha kuwa matumizi ya hatifungani za makampuni kwa miradi ya miundombinu yameongeza ufanisi wa uwekezaji kwa **asilimia 25** katika nchi za SADC.
- iii. **Usimamizi thabiti wa sekta ya fedha nchini;** Serikali inahitaji kuimarisha na kuboresha mifumo ya kifedha nchini ili kuhakikisha sekta binafsi ya ndani inapata nafasi ya kushiriki kikamilifu katika miradi ya maendeleo ili kupunguza utegemezi wa mitaji ya nje pekee. Hii inajumuisha kuimarisha taasisi za kifedha, kuongeza upatikanaji wa mikopo nafuu, na kuendeleza masoko ya mitaji ya ndani.
- iv. **Serikali kufungua soko la mitaji polepole;** Tafiti za Benki ya Dunia (World Bank, 2023) na Shirika la Fedha Duniani (IMF, 2024) zinaonyesha kuwa nchi ambazo zimefungua masoko ya mitaji polepole zimefanikiwa kuongeza Mahitaji kutoka nje (FDI) kwa wastani wa **asilimia 2–3** ya GDP ndani ya miaka mitano ya kwanza, huku zikidumisha uthabiti wa kifedha. Hivyo, ni muhimu Serikali ikazingatia ni namna gani inalitekeleza hili na kwa uharaka gani ili kuhakikisha kuwa linafikia matarajio iliyojiwekea.

**Mheshimiwa Spika**, iwapo masuala hayo yatazingatiwa ni dhahiri kuwa malengo ya Serikali ya kuongeza mitaji kutoka nje (FDI) hadi **≥10%** ya GDP kufikia 2030 yatafikiwa na hivyo sekta binafsi kuwa injini ya utekelezaji wa Dira ya 2050.

#### **5.5. Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kuajiri na kuwawajibisha watumishi wake**

**Mheshimiwa Spika**, Mamlaka ya Mapato ya Tanzania ilianzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Mapato, Sura 399. Aidha, kifungu cha 21 cha Sheria hiyo imeipa TRA mamlaka na uhuru wa kuajiri na kushughulikia masuala ya kiutumishi yanayowahusu watumishi wake. TRA imekuwa ikitumia mamlaka hayo tangu kuanzishwa kwake mwaka 1996 hadi Julai 2019 ambapo Mamlaka hayo yaliondolewa kwa tamko la ujumla la serikali. Kufuatia mabadiliko hayo, Mamlaka imekuwa na changamoto ya uwezo wa kuajiri na kufuta kazi watumishi hasa kwa utovu wa nidhamu na ubadhilifu mpaka ipate idhini kutoka Utumishi wa Umma, hali ambayo imekuwa ikisababisha baadhi ya watumishi kuhamishwa wakati walistahili kufukuzwa na wengine kurejeshwa kazini ilihali Mamlaka ilitaka wafukuzwe.

**Mheshimiwa Spika**, katika kukabiliana na changamoto hiyo, Mamlaka ilichukua hatua ya kumuandikia Katibu mkuu utumishi barua yenye kumb. Na. CFC.26/205/01/AT/TEMP56 ya tarehe 17 Februari 2023, ili kuomba idhini ya kuajiri na kufuta kazi watumishi kwa utovu wa nidhani. Kwa kuzingatia unyeti wa Mamlaka ya Mapato Tanzania katika kuwezesha serikali kutimiza malengo yake, hususani katika ukusanyaji wa mapato, ombi la TRA liliridhiwa na hivyo, kuendelea na utaratibu uliokuwa ukitumika kwa mujibu wa Sheria ya Mapato Tanzania. Vilevile, Tume ya Mh. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mapitio ya sheria za kodi pamoja na mapendekezo mengine ilitoa la pendekezo

la kurekebisha vifungu vya 35, 36, na 37 vya Sheria ya Utumishi wa Umma, Sura 298 ili kuipa TRA Mamlaka Kamili ya kuchukua hatua za kinidhamu, ikiwemo kufukuza Watumishi wake inapobidi na kuiondoa kwenye utaratibu wa Sheria za Utumishi wa Umma.

**Mheshimiwa Spika**, katika kuhakikisha kuwa maelekezo ya kuridhiwa na kurejeshwa mamlaka hayo kwa TRA na kuweza kutekelezeka bila kuwepo kwa vikwazo vyovyote kisheria, sambamba na pendekezo tajwa la tume ya Rais ya mapitio ya sheria za kodi, Kamati inapendekeza kufanyiwa marekebisho ya kifungu cha 10 cha sheria ya Utumishi wa Umma, Sura 298 ili kuiongeza Mamlaka ya Mapato Tanzania kwenye orodha na kuwa mojawapo ya taasisi nyeti zisizo athiriwa na matakwa ya kifungu hicho. Kwakuwa mabadiliko haya yanawahusu TRA ikiwa ni taasisi inayohusika na makusanyo ya Mapato ya Serikali, Kamati inaitaka Serikali kuwasilisha mabadiliko ya Sheria hizo kupitia Sheria ya fedha ya mwaka 2026.

## **6.0. HITIMISHO**

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuhitimisha kwa kukushukuru wewe Mhe. Mussa Azzan Zungu, Mb Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Mhe. Daniel Baran Sillo, Mb Naibu Spika kwa kuendelea kuliongoza vema Bunge. Nawashukuru pia Mhe. Bal. Khamis Mussa Omar, Mb Waziri wa Fedha, Mhe. Mshamu Ali Munde, Mb Naibu Waziri wa Fedha na Mhe. Laurent Deogratius Luswetula, Mb Naibu Waziri wa Fedha, kwa ushirikiano wao wakati wa kuchambua utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2025/26 na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2026/27. Aidha, napenda kumshukuru Dkt. Natu El-Maamri Mwamba, Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mlipaji Mkuu wa Serikali, Manaibu Katibu Wakuu, Wakuu, Kamisha wa Bajeti, Taasisi na Idara zote zilizo chini ya Wizara ya Fedha pamoja na Wataalamu wote wa Wizara ya Fedha kwa ushirikiano wao katika

kujadili, kuchambua na kupitisha makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara.

**Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya pekee napenda kumshukuru Ndg. Charles Kichere Mdhiniti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa ushirikiano wake kwa Kamati wakati wa kujadili utekelezaji wa majukumu ya Ofisi yake kwa mwaka 2025/26 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2026/27.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwapongeza wajumbe wa Kamati kwa umahiri, umakini na ushirikiano wao walionipatia wakati wote wa kupitia na kuchambua bajeti ya Wizara hii na hatimaye kukamilika kwa Taarifa hii. Naomba kuwatambua Wajumbe hao kama ifuatavyo: -

1. Mhe. Mashimba Mashauri Ndaki, Mb Mwenyekiti
2. Mhe. Ali Hassan Omar King, Mb Makamu Mwenyekiti
3. Mhe. Bal.Dkt. Pindi Hazara Chana, Mb Mjumbe
4. Mhe. Hussein Mohamed Bashe, Mb Mjumbe
5. Mhe. Innocent Lugha Bashungwa, Mb Mjumbe
6. Mhe. Esther Nicholas Matiko, Mb Mjumbe
7. Mhe. Amina Idd Mabrouk, Mb Mjumbe
8. Mhe. Stella Alex Ikupa, Mb Mjumbe
9. Mhe. Joseph Zacharius Kamonga, Mb Mjumbe
10. Mhe. Bahati Kenneth Ndingo, Mb Mjumbe
11. Mhe. Ally Yahya Mhata, Mb Mjumbe
12. Mhe. Kakulu Buchard Kakulu, Mb Mjumbe
13. Mhe. Dkt. Catherine Canute Joachim, Mb Mjumbe
14. Mhe. Moses Charles Bujaga, Mb Mjumbe

- |   |        |
|---|--------|
| 15. Mhe. Asma Ali Mwinyi, Mb            | Mjumbe |
| 16. Mhe. Haran Nyakisa Sanga, Mb        | Mjumbe |
| 17. Mhe. Devotha Daniel Mburarugaba, Mb | Mjumbe |
| 18. Mhe. Thomas Mgonto Kitima, Mb       | Mjumbe |
| 19. Mhe. Enock Zadock Koola, Mb         | Mjumbe |
| 20. Mhe. Nancy Hassan Nyalusi, Mb       | Mjumbe |

**Mheshimiwa Spika**, mwisho si kwa umuhimu, nimshukuru Ndg. Baraka Leonard Katibu wa Bunge kwa niaba ya Watumishi wote kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kikamilifu pamoja na kutoa ushauri wa kitaalamu uliowezesha kufanikisha shughuli za Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo naliomba Bunge lako Tukufu sasa lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mafungu nane (8) ya Wizara ya Fedha pamoja na Fungu 45 la Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2026/27 kama yalivyowasilishwa na Waziri wa Fedha yenye jumla ya **Shilingi 21,520,609,384,000** ambapo **Shilingi 809,120,054,000** ni mishahara, **Shilingi 18,760,164,179,000** ni matumizi mengineyo na **Shilingi 1,951,325,151,000** ni matumizi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

  
Mhe. Mashimba Mashauri Ndaki (Mb)  
**MWENYEKITI**

**KAMATI YA BUNGE YA BAJETI**

02 Juni, 2026